HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE: JAJI MSTAAFU DAMIANI LUBUVA KATIKA MKUTANO WA TUME NA VYOMBO VYA HABARI UNAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA TUME, TAREHE 28/07/2015.

Waheshimiwa Wajumbe wa Tume,
Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Watendaji wa Tume,
Waandishi wa Habari,

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisheni wote katika mkutano huuwa kupeana taarifa kuhusu zoezi la Uandikishaji wa Wapiga Kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Tunatambua kuwa mna majukumu mengi na ya muhimuna hasa muda huu ambapo wengi wenu mlitakiwa kuwa katika Vyumba vyenu vya

Habari kwa ajili ya kuandaa taarifa mbalimbali za leo lakini mmetambua umuhimu wa mkutano huu na mmeweza kufika.

Asanteni sana.

Ndugu Wanahabari,

Mnatambua kuwa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linaendelea katika jiji la Dar es salaam na hii leo limeingia katika siku ya saba. Zoezi hili la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mkoa wa Dar es salaam lilianza rasmi tarehe 22 Julai 2015 na linatarajiwa kukamilika tarehe 31 Julai 2015.

Kama ambavyo tumekuwa tukiwaahidi Wadau wa Uchaguzi mara kwa mara kuwa Tume itakuwa ikitoa taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika zoezi hili, leo Tume inakutana nanyi kuwapa taarifa ya maendeleo ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Lengo ni kuhakikisha kuwa zoezi hili la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linafanyika kwa ufanisi na linafanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakutana nanyi muda huu baada ya kujitokeza kwa masuala ya dharura ambayo sisi kama Tume tumeona ni

vema tuyatolee ufafanuzi ili kuhakikisha kuwa zoezi hili kwa Mkoa wa Dar es salaam linafanyika na kukamilika

Ndugu Waandishi wa Habari,

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unahusisha pia kuandikisha Wapiga Kura wote waliotimiza umri wa kumi na nane (18) au zaidi na wale ambao ifikapo siku ya upigaji wa Kura ya Maoni na Uchaguzi Mkuu wa 2015 watakuwa wametimiza umri wa miaka 18. Zoezi hili vilevile, litahusisha wale wote ambao kwa sababu mbalimbali hawakuwahi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika mazoezi yote ya uandikishaji yaliyopita. Baada ya zoezi la Uandikishaji kukamilika, Daftari la Awali la Wapiga Kura litawekwa wazi katika maeneo husika na tarehe za kukagua Daftari na kusahihisha taarifa za Mpiga Kura zilizokosewa zitatangazwa na Tume kusudi kila aliyejiandikisha aende kukagua na kujiridhisha kuwa taarifa zake zimeandikwa kwa usahihi.

Kipindi cha kuweka wazi Daftari la Awali pia kinatoa fursa kwa Wapiga Kura waliojiandikisha ndani ya Kata kuweka pingamizi kwa wale ambao wataonekana wameandikishwa katika Daftari lakini hawana sifa mfano

wasiokuwa raia au wasiotimiza umri unaotakiwa. Baada ya kuweka wazi Daftari la Awali, Tume itachapisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa wito kwa wananchi wote wenye sifa za kujiandikisha kujitokeza kwa wingi katika vituo vyote vya uandikishaji na kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Ni vyema ieleweke kwamba Mpiga Kura aliyejiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la sasa na kupewa kadi ya Mpiga Kura, ndiye atakayeruhusiwa kupiga Kura.

Wakati wa uandikishaji kipaumbele kitatolewa kwa watu wanaoishi na Ulemavu, Wazee, Wagonjwa, Akinamama Wajawazito na wale wenye watoto wachanga hawatalazimika kusimama kwenye mstari bali wataruhusiwa kuingia kituoni na kujiandikisha.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Tume kwa upande wake imejiandaa vyema ili kuhakikisha kuwa shughuli zote zinazoonyeshwa kwenye ratiba zinafanyika kwa muda uliopangwa

ikiwa ni pamoja na kufikisha vifaa vya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika maeneo husika kwa muda uliopangwa.

Vyombo vya Habari ni sehemu ya jamii na vina nafasi kubwa ya kutoa mchango na kushiriki katika mchakato mzima wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kuwa mko karibu na wananchi na mnayo taaluma ya namna ya kufikisha habari kwenye maeneo mbalimbali ya nchi.

Kupitia Vyombo vya Habari wananchi wanaweza kuelimishwa na kuhamasishwa kushiriki katika mchakato wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuona kila raia mwenye sifa anaandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na hatimaye kushiriki katika Uchaguzi. Tume inaviomba Vyombo vya Habari kuelimisha raia kujua haki yao hiyo ili wajitokeze kujiandikisha. Kwa kuwa zoezi hili la Uboreshaji linatumia Teknolojia mpya ya BVR, inahitajika wananchi kuelimishwa na kuhamasishwa kwa kiwango kikubwa na kupewa taarifa sahihi za Uboreshaji. Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa upande wake imejiandaa vyema kuhakikisha kuwa zoezi hili linaendeshwa kwa ufanisi mkubwa. Vilevile, imeandaa mkakati wa utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kwa kutumia njia mbalimbali za kutoa elimu ikiwemo Vyombo vya Habari.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kwa kumalizia, ninapenda tena kuwashukuru wote kwa kuhudhuria mkutano huu. Ombi letu kwenu ni kuwataka kusaidia kufikisha taarifa hizi kwa umma kwa usahihi na zaidi sana kuhamasisha watu waweze kujitokeza kwa wingi kwenye zoezi hili.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA